# Ujumbe wa Jenerali wa Pasaka ya Mwaka 2023

## 'Imekwisha' (Yohana 19:30)

Pasaka hii inakuja wakati viongozi wote wa Jeshi la Wokovu kote duniani wameitwa waje pamoja kumchagua Jenerali mpya. Upendeleo wa kutumika katika ngazi ya viongozi wa kimataifa sasa unafikia mwisho kwa Komishena Rosalie nami, na tunahitaji kukamilisha kile tulichoamua kukifanya. Hivi karibuni tutahitaji kusema, 'Imekwisha'.

Kwa hiyo ninapotafakari kuhusu Pasaka, navutwa na maneno ya Yesu msalabani: 'Imekwisha'. Lakini neno hilo kutoka katika kinywa cha Yesu lina uzito kiasi gani kama lilivyorekodiwa katika Yohana 19:30. Maisha na huduma yake ya hapa duniani – maisha ya kibinadamu yaliyo bora kuliko yote na huduma iliyosambaa zaidi kuliko zote – ilikamilika.

*Imekwisha.*

Lakini neno 'Imekwisha' lina maana ya kina zaidi tunapofikiria kwamba Yesu alilisema katika lugha yake ya Kiebrania, kwahiyo neno alililotumia linaonyesha kujitoa kikamilifu – kulikokamilika kabla hajafa. Katika Kristo, Mungu ambaye alikuwa hawezi kufa, kwa hiari yake na kikamilifu alijitoa akawa mwanadamu. Kwa kufanya hivyo alipata maumivu, mateso na kifo chenyewe. Paulo anayaelezea haya katika Wafilipi 2:5-8 anapoandika akisema, 'Iweni na nia hiyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwemo pia ndani ya Kristo Yesu; ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu, tena alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam mauti ya msalaba.' Yesu alijivika ubinadamu wetu. Alitufahamu. Alipitia mateso yaliyokithiri ya mauaji ya hadharani na unyanyasaji wote. Alijitambulisha akafanana nasi katika uzoefu wa kibinadamu – ikiwa pamoja na machungu, mateso na kifo – anasimama aliyekamilisha.

*Imekwisha.*

Yohana alipoandika baadaye Injili yake kwa Kiyunani, aliweka kumbukumbu 'Imekwisha' kama maneno ya mwisho ya Yesu, akitumia neno kutoka katika ulimwengu wa fedha linalomaanisha, 'imelipwa kikamilifu'. Kwa hiyo Mwinjilisti anatukumbusha kwamba, katika Yesu, kujitoa kikamilifu, alilipa deni la dhambi kwa binadamu wote. Pale msalabani deni letu limelipwa kikamilifu. Paulo anaunganisha 'malipo kikamilifu' na dhambi zetu hazihesabiwi tena na msisitizo muhimu wa upatanisho kupitia kwa msalaba. Analielezea hili katika 2 Wakorintho 5:19: 'Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao, naye ametia ndani yetu neno la upatanisho.' Dhambi tena sio swala – jambo muhimu ni namna gani tutamwitikia Mwokozi aliyetulipia deni letu kikamilifu.

*Imekwisha.*

Mwanzo wa mwaka, nilimthibitisha **'Mungu wa mara moja tu**.' Katika Warumi 6:10 tunasoma: 'Maana kwa kule kufa kwake, aliifia dhambi mara moja tu; lakini kwa kule kuishi kwake, amwishia Mungu.' Msaada wa Mungu kwetu ulianza na agano jipya, nalo likaanza na msalaba. Mara moja tu. Akalipa kikamilifu. Waebrania 9:28 inatukumbusha kwamba Kristo alitolewa sadaka mara moja ili azichukue dhambi za wengi, pamoja na sisi, wakati Yohana 1:29 inatangaza kwamba, 'Tazama mwanakondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu'. Hiyo ni dhambi yangu na yako.

*Imekwisha.*

Ndani ya ukweli kwamba Kristo alikufa mara moja tu, kuna ukweli vile vile kwamba anaishi, na kwasababu anaishi, sisi tunaweza kuishi vile vile. Hiki ndicho kiini cha ujumbe wa Pasaka. Haijalishi nini kitatokea, ukweli wa tendo la Mungu kwa niaba yetu unabaki kuwa mwamba ulio imara. Haijalishi nini kitakuja sisi tunabakia salama mikononi mwake na tunatambua kikamilifu msaada wake. Haijalishi nini kitatokea, tunaweza kuishi kama 'zaidi ya washindi' katikati ya mambo yote', kwasababu neema yake yatosha naye ni mwaminifu. Warumi 5:8 inasema: 'Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu tulipokuwa tungali wenye dhambi.' Imekwisha! Mara moja tu…..na hilo lilibadilisha kila kitu.

*Imekwisha.*

Kamishena Rosalie anaungana nami kuwatumieni salaam zenye uvuguvugu za Pasaka.

**Brian Peddle**
**Jenerali**